JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Shule ya Sekondari IWAWA

S.L.P, 33

Tarehe 13.06.2023

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA **TANO** KATIKA SHULE YA **SEKONDARI IWAWA** HALMASHAURI YA WILAYA **MAKETE** MKOA NJOMBE MWAKA **2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari **IWAWA** ipo umbali wa Kilometa 112 Magharibi mwa Mji wa NJOMBE na umbali wa Kilometa 84 kutoka Mbeya mjini, Usafiri wa basi kutoka Njombe mjini unapatikana stendi kuu ya **NJOMBE** na Mbeya mjini utapandia kituo cha mabasi cha **UYOLE** Nauli ni Shilingi 10,000/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 13.08.2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13.08.2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31.08.2023**



Edit with WPS Office

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni suruali mbili za heshima zisizobana, suruali moja rangi ya damu ya mzee na suruali ya pili rangi ya mastadi
ii. Mashati mawili au zaidi meupe yenye mikono mirefu.
iii. Sare ya Michezo ni tracksuit jozi mbili nyeusi pana isiyobana na yenye mistari mitatu myeupe ya kunyooka, pamoja na raba za rangi ya aina yoyote ile zisizo na njumu.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili au zaidi za rangi nyeusi.
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wenye ulimi kwenye kishikizo wa kuvalia suruali;
vii. Sweta mbili au zaidi kwani kuna baridi rangi ya bluu;
viii. Tisheti (T-shirt) rangi ya njano inapatikana jirani na shule.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari counter book 10 za QUIRE 3;
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo utanunua kulingana na tahsusi ( combination ) uliyochaguliwa;
iv. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa mchepuo wa EGM, HGK na HGL;
v. Godoro lenye upana wa nchi $2^{1}/2$ X 4 X 6;
vi. Mashuka Jozi 2 moja rangi ya bluu bahari ( light blue ) na la pili rangi ya pink , blanket zito 1 na foronya ya godoro ( bed cover ) 1*;*
vii. Jaketi jeusi zito lisilo na kofia nyuma na maandishi ya aina yoyote kwa ajili ya kujisitiri na baridi wakati wa jioni;
viii. Nguo za ndani za kutosha, Taulo na ndala za kuogea.
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1 iliyonolewa, jembe 1 lenye mpini lililonolewa, mopa 1 na brush 1 mfagio wa chelewa 1 na brash ndogo ya kusugulia sinki za chooni ( kishungi ) kwa ajili ya usafi wa mabwenini,



Edit with WPS Office

madarasani na nje kwenye mazingira ya shule.

xii. Flat file 1 kwa ajili ya kutunzia taarifa za mwanafunzi.

### 2.3 Michango mbalimbali

**Hii ni Shule ya Bweni michango ni kama ifuatavyo;**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo ya shule | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango hii iwekwe kwenye akaunti ya shule NMB 60401100031 JINA: IWAWA SECONDARY SCHOOL ACCOUNT**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku( Night Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;



Edit with WPS Office

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

- **Matibabu ya MTOTO NI JUKUMU LA MZAZI NA SI LA SHULE (mzazi utajulishwa kuhusu afya ya mtoto wako)**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale



Edit with WPS Office

yanayovunja sheria za nchi;

xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule; 0754991887
- Makamu Mkuu wa Shule; 0759743302
- Mwandamizi Taaluma; 0710863300
- Mwandamizi Malezi; 0768359573
- Patron: 0716940461

Saini ya Mkuu wa Shule……………………………

Jina la Mkuu wa Shule; ......................................................

Mhuri wa Mkuu wa Shule......................................................../.



Edit with WPS Office

## 4. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI.
### 4.1 AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi…………………………………………………………………..Mzazi/Mlezi wa ……………………..…………..…………………(jina la mtoto) ninakubali mwanangu aje Shule ya Sekondari Iwawa na ninaahidi kumtimizia mahitaji yote yaliyoagizwa. Pia naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule kumlea na kumtunza kwa maadili ya Ki–Tanzania (awapo Shuleni na likizo ) mpaka atakapo maliza masomo yake. ***Aidha Sitampa Mwanangu Simu Muda Wote Awapo Shuleni wala mavazi nje ya sare ya shule iliyoagizwa. Mawasiliano yangu yote nitayafanya kupitia Uongozi wa Shule.***
Na kama kuna mabadiliko nitautarifu Uongozi wa Shule.

Anuani yangu ya kudumu: ………………………………………namba ya simu……………………….……
Sahihi. ………………………………Tarehe ……………………….

**Walezi watakao kuja kumwona mwanafunzi ni;**

| | | |
|---|---|---|
| 1……………………………simu……… ………………. | 2……………………………...simu…… ……………….. | 3……………………………..simu……… ………………….. |
| bandikapicha | bandikapicha | bandikapicha |

### 4.2 AHADI YA MWANAFUNZI.

Mimi……………………………….……………………………………….Nakubali/Sikubali* Nafasi niliyopewa katika Shule ya Sekondari ya Iwawa. Naahidi kuwa nitazitii Sheria zote za Shule na kufuata maelezo na maagizo yote nitakayopewa na Mkuu wa Shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa Serikali ya Wanafunzi.

***Aidha sitakuwa na simu muda wote niwapo shuleni wala kuwa na mavazi nje ya sare ya shule niliyoagizwa. Pia sitashiriki katika migomo au kuhamasisha migomo, fujo na makosa ya jinai***

Shule niliyo soma ni ……………………………….………………… Namba ya Mtihani ni ………...
Sahihi …….……………………. Tarehe ……………………………

### *5. SEHEMU YA MGANGA .*



Edit with WPS Office

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**MAKETE DISTRICT COUNCIL**

**IWAWA SECONDARY SCHOOL**

**(REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION)**

This form must be completed by a Government Medical Officer

Name of Student ....................................................................................................

Age ............................................................ Sex .....................................................

The above named pupil has been examined in respect of

a) PREGNANCY TEST (FOR GIRLS ONLY) ..............................................................
b) STOOL ...................................................................................................
c) URINE ...................................................................................................
d) CHEST ...................................................................................................
e) BLOOD ...................................................................................................
f) EYES ...................................................................................................
g) EARS ...................................................................................................
h) OTHER FINDINGS .........................................................................................
   .........................................................................................
   .........................................................................................

I am satisfied that the above named pupil is fit/not fit for pursuing Secondary studies at IWAWA SECONDARY SCHOOL.

................................................ ......................................

**SIGNATURE** **DATE**

..................................................... ...........................................

**DESIGNATION and OFFICIAL STAMP** **STATION**

**Mhuri wa Mkuu wa** **Shule...........................................**



Edit with WPS Office



Edit with WPS Office



Edit with WPS Office